# Pua La Ngamia

**na**

**Ellis P. Forsman**

# Pua La Ngamia

**na**

**Ellis P. Forsman**

**Oktoba 14, 2011**

# Pua La Ngamia

## Yakobo 1:17-27

Alexander Campbell wakati fulani alitoa adithi ya ngamia aliyetaka pua lake pekee liwe katika mlango wa hema – pua lake pekee, hakuna cha zaidi – alitaka tuu apate harufu nzuri ya iliyotokea ndani ya hema ile. "Tafadhali ruhusu tu pua langu." Hata ivyo hiyo haikumridhisha ngamia. Ghafla akaanza kupasha joto manyoya yake, nundu na vyote, ndani ya hema, na kama watu waliokuwemo ndani hawakuipenda, walipaswa kutoka nje. Ngamia alitaka kuishi ndani ya hema lile.

Alexander Campbell akasema ngamia huyu ana majina mengi katika dini – cho chote ambacho hakijaruhusiwa katika maandiko ya Agano Jipya ambayo yanapaswa kuzingatiwa – ruhusu tu na uwe na mawazo mapana; alafu mara sema kweli, "Unafanya nini hapa?"

Wakati vuguvugu la urejesho, Alexander Campbell alishikilia kwamba ngamia huyu alipaswa kufukuzwa na sio kumruhusu aingize pua lake katika kanisa. Alishikilia ukweli wa Biblia kwamba ndiyo yanapaswa kuwa na mamlaka na ya kwamba mawazo ya kibinadamu hayapaswi kuwa na sehemu katika dini.

## Pua la ngamia katika dini

Katika historia ya kanisa kumekuwa na ngamia wengi ambao ghafla wanataka pua zao ziwe katika mlango wa hema.

Jamii ya wamishionari na jamii zingine, makundi na mashirika, vyombo vya mziki, watu wa vikombe vingi, shule za juma pili, wahubiri walioajiriwa, wanawake waalimu, ushirika wa wazi (hii ni kumuita mtu ye yote ili tu ashiriki katika sehemu fulani ya huduma ya kanisa bila kujali dini zao (awe hajabatizwa, mwenye dhambi ambaye hajatubu (mfano uliotolewa: mtu aliyebatizwa, alafu baadaye akajiingiza katika mafundisho ambayo siyo ya kibiblia) n.k)).

Yak. 1:17-27, "*Kila kutoa kuliko kwema, na kila kitolewacho kilicho kamili hutoka juu hushuka kwa Baba wa mianga; kwake hakuna kubadilika wala kivuli cha kugeuka geuka. Kwa kupenda kwake mwenyewe alituzaa sisi kwa neno la kweli, tuwe kama limbuko la viumbe vyake. Hayo mnajua ndugu zangu wapenzi. Basi kila mtu na awe mwepesi wa kusikia, bali si mwepesi wa kusema; wala kukasirika; kwa maana hasira ya mwanadamu haitendi haki ya Mungu. Kwa hiyo wekeni mbali uchafu wote na ubaya uzidio, na kupokea kwa upole neno lile lililopandwa ndani liwezalo kuziokoa roho zenu. Lakini iweni watendaji*

*wa neno wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu. Kwa sababu mtu akiwa msikiaji wa neno tu, wala si mtendaji mtu huyo ni kama mtu anayejiangalia uso wake katika kioo. Maana hujiangalia kisha huenda zake, mara akasahau jinsi alivyo. Lakini aliyeitazama sheria kamilifu iliyo ya uhuru, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu, bali mtendaji wa kazi huyo atakuwa heri katika kutenda kwake. Mtu akidhani ya kuwa anayo dini wala hauzuii ulimi wake kwa hatamu, hali akijidanga wake, dini yake mtu huyo haifai. Dini iliyo safi isio na taka mbele na Mungu Baba ni hii, kwenda kuwatazama yatima na wajane katika dhiki yao, na kujilinda na dunia pasipo mawaa.*"

Watu wa kisasa ni kama ngamia anayetaka tu pua lake liwe katika mlango wa hema.

# Uhuru – kilio cha kisasa

Gal. 5:1, "*Katika ungwana huo Kristo alituandika huru, kwa hiyo simameni wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.*"

Uhuru aimanishi ruhusa ya kufanya cho chote ambacho mtu anataka kufanya.

Hakuna mchanganyiko kati ya uhuru na sheria.

Neno la mwisho la "Mwamerika Mzuri" – "uhuru wako ni sheria." Uhuru unapatikana katika mamlaka.

Mamlaka yanahakikisha uhuru wa kuishi bila kuogopa machafuko. Pasipo mipaka na ukomo kusingekuwa na uhuru.

Mtunzi wa zaburi, Daudi hakuona mkanganyiko kati ya uhuru na sheria katika Zab. 119:44-45, "*Nami nitaitii sheria yako daima, naam, milele na milele. Nami nitakwenda panapo nafasi, kwa kuwa nimejifunza mausia yako.*"

Yak. 1:25, "*Lakini aliyeitazama <u>sheria kamilifu iliyo ya uhuru</u>, na kukaa humo asiwe msikiaji msahaulifu bali mtendaji wa kazi, huyo atakuwa heri katika kutenda kwake.*"

## Uhuru unamaanisha kutofungwa na kitu fulani, lakini kutoka katika nini?

**Kutoka katika utumwa wa Sheria ya Kale.**

Rum. 8:2-3, "*Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu dhambi katika mwili;*"

**Kutoka katika utumwa wa dhambi zetu wenyewe.**

- Yoh. 8:34, "*Yesu akajibu akawaambia, Amin, amin, nawaambia, kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi.*"
- Rum. 6:16, "*Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki.*"
- Rum. 6:18, "*Na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.*"

Haki ya Mungu, siyo yetu.

Mtume Paulo hakuona tofauti kati ya uhuru na utii.

Ni uhuru upi ambao Gal. 5:1 inazungumzia?

Gal. 5:1, "*Katika ungwana huo Kristo alituandika huru, kwa hiyo simameni wala msinaswe tena chini ya kongwa la utumwa.*"

Jibu lipo katika msitari ufuatao. Gal. 5:2, "*Tazama mimi Paulo nawaambia ninyi ya kwamba, mkitahiriwa Kristo hatafaidia neno.*" Maagizo ya Sheria ya Kale.

Je tupo katika uhuru wa kufanya cho chote tunachokitaka?

Mungu anasema nini kuhusiana na vitu vya dunia kuwa huru?

2 Pet. 2:19-20, "*Wakiwahidia uhuru, nao wenyewe ni watumwa wa uharibifu, maana mtu akishindwa na mtu huwa mtumwa wa mtu yule. Kwa maana wale waliokwisha kuyakimbia machafu ya dunia kwa kumjua Bwana na Mwokozi Yesu Kristo, kama wakinaswa tena na kushindwa, hali yao ya mwisho imekuwa mbaya kuliko ile ya kwanza.*"

Nia yetu inapaswa iweje kuhusiana na uhuru wetu?

1 Pet. 2:13 -16, "*Tiini kila kiamriwacho na watu, kwa ajili ya Bwana ikiwa ni mfalme, kama mwenye cheo kikubwa; ikiwa ni wakubwa kama wanaotumwa naye ili kuwalipiza kisasi watenda mabaya na kuwasifu watenda mema. Kwa sababu ndiyo mapenzi ya Mungu, kwamba kwa kutenda mema mzibe vinywa vya ujinga vya watu wapumbavu; kama walio huru, ila wasiotumia uhuru huo kwa kusitiri ubaya, bali kama watumwa wa Mungu.*"

Kama ndugu yetu anahisi kwamba kitu fulani ni dhambi, tunapaswa kukiacha kwa ajili yake (ikiwa tu inaingilia sheria ya Mungu).

1 Kor. 8:13, "*Kwa hiyo chakula kikimkwaza ndugu yangu hakika sitakula nyama hata milele, nisije nikamkwaza ndugu yangu.*"

# Watu wa kisasa wanalilia "roho, siyo barua ya sheria"

2 Kor. 3:6, "*Naye ndiye aliyetutosheleza kuwa wahudumu wa agano jipya; si wa andiko bali wa roho; kwa maana andiko huua, bali roho huhuisha.*"

Watu wa kisasa wanasema, "kile ambacho kifungu hiki kinasema siyo muhimu kuliko roho iliyoko nyuma yake." Hii inatulainisha ili tupotee.

Hiki ndiyo kilisababisha mgawanyiko wote wa kidini ambao Campbell alizungumzia.

Njia pekee ya kutambua roho ya agizo ni kupitia katika barua ya agizo. Kama barua ni ya uongo, au siyo muhimu, hakuna njia yo yote ya kutambua roho ya agizo ilivyo. Kama hakuna barua, pia hakuna mamlaka. Kila mmoja wetu, basi, yuko huru kuamua roho yake.

Kama barua inaua, basi ubatizo nao unaua? Kama watu wa kisasa wako sahihi, basi ni makosa kutii waraka au barua.

Ingeweza kuua maisha ya kiroho kushiriki Meza ya Bwana, maana mkate na uzao wa mzabibu uitangaza barua au waraka.

Kifungu cha 2 Kor. 3:6 aihusiani na ndani na nje ya agano jipya, bali ya Agano la Kale na Agano Jipya.

2 Kor. 3:7-9, "*Basi ikiwa huduma ya mauti iliyoandikwa na kuchorwa katika mawe, ilikuja katika utukufu hata Waisraeli hawakuweza kuukazia macho uso wa Musa, kwa sababu ya utukufu wa uso wake; nao ni utukufu ulikuwa ukibatilika; je! Huduma ya roho haitazidi kuwa katika utukufu? Kwa maana ikiwa huduma ya adhabu ina utukufu, siuze huduma ya haki ina utukufu unaozidi.*"

Mtume Yohana anaisema vyema: Yoh. 4:24, "*Mungu ni Roho nao wamwabuduo imewapasa kumwabudu katika roho na kweli.*"

Wayahudi walikuwa na neno la Mungu, lakini hawakuishi kwa Roho.

## Ngamia wanaanzia katika kusanyiko

Hiki ni kitu ambacho tunatakiwa kuwa nacho makini. Haiwezi kuzuilika kirahisi hadi iwe na nguvu. Ni pua tu kupita katika mtikisiko.

Nukuu kutoka kwa R. C. Lenski, "Mwanzoni ukengeufu unanyenyekea na kuomba kuruhusiwa. Inaomba kufunguliwa akili. Hataivyo, ikisha ruhusiwa inapanuka, na kwa dhihaka inauliza ukweli: "Unafanya nini hapa?"

Mwalimu wa uongo hawezi kuonekana kuwa anavutia kwa mara ya kwanza; lakini asipo chunguzwa, atawavuta wengine hadi kuwaweka katika mawazo yake ya kisasa na hii inajenga tatizo katika kanisa.

Mara nyingi hawa watu wa kisasa wanafikiria filosofia, alafu wanaanza kuchanganua Biblia kulingana na filosofia yao, badala ya kufanya Biblia kuwa kiwango cha kuongoza fikira zetu.

Lenski anasema, "Tatizo moja la linalotokea unapokabiliana na hawa watu wa kisasa ni kwamba kunakuwa na udhaifu wa wazi miongoni mwao na wanakuta kuwa ni vigumu kuwapinga watu wema wanaofundisha mafundisho ya uongo. Wapo wengi wanaofanana, waalimu wazuri wanaofundisha elimu ya uongo katika ulimwengu leo.

- 2 Tim. 4:3-4, "*Maana utakuja wakati watakapoyakataa mafundisho yenye uzima, ila kwa kuzifuata nia zao wenyewe watajipatia waalimu makundi makundi, kwa kuwa wana masikio ya utafiti; nao watajiepusha wasisikie yaliyo kweli, na kuzigeukia hadithi za uongo.*"

- Gal. 1:6-9, "*Nastajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi injili yo yote, isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaniwe. Kama tulivyokwisha kusema na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea na alaaniwe.*"

- Rum. 16:17-18, "*Ndugu zangu nawasihi waangalieni wale wafanyao fitina na mambo ya kukwaza kinyume na mafundisho mliyojifunza, mkajiepushe nao. Kwa sababu walio hivyo hawamtumikii Bwana wetu Kristo, bali matumbo yao wenyewe; na kwa maneno laini na ya kujipendekeza wataidanganya mioyo ya watu wanyofu.*"

Wakati fulani nilisoma jarida la kanisa la makanisa ya Kristo yaliyopotoka ambayo ilitaja kanisa moja ambalo lilikuwa na tatizo ambapo mtu mmoja alikuwa akiwatembelea na kutaka kupoteza vijana wao.

Mtu huyu ghafla aliwekwa katika nafasi ya kufundisha vijana wao katika kundi. Kijana mmoja aliyehudhuria darasa hili akamwambia wazazi wake kwamba mtu huyo alikuwa anafundisha darasa kwamba ubatizo siyo muhimu kwa ajili ya wokovu. Wazazi wakapeleka habari hii kwa mmoja wa wazee wa kanisa, ambaye mwanzoni aligundua kwamba mtu huyo hafundishi uongo. Hataivyo, alikubali kufanya uchunguzi.

Juma pili iliyofuata, muda mfupi baada ya wanafunzi kwenda katika madarasa yao, mzee huyo akaingia katika darasa la vijana ili kuona ghafla mwalimu huyu akawa anajitahidi ili afiche nyaraka alizokuwa akifundishia. Mwalimu huyu aliliambia darasa kwamba, "Leo tutajifunza kitu tofauti." Mzee huyo aliomba kuangalia nyaraka ambazo mwalimu huyo aliweka pembeni na akapata kwamba habari ambayo wazazi walimpelekea ilikuwa ni kweli. Mzee akaliambia darasa kwamba hataruhusiwa kufundisha tena.

Wanataka waruhusiwe (au kama ilivyo katika shauri hili, wanadanganya); alafu wanataka kupotosha; alafu wanataka kutawala.

Nukuu kutoka kwa J. Robertson McQilkin, "Upotofu wa mafundisho katika kundi kidogo uanza kwa kukataa mafundisho muhimu bali kwa tofauti ya fundisho hilo. Mkanganyo mara nyingi huanza wakati wa ukimya.

2 Thes. 2:15, "*Basi ndugu simameni imara mkayashike mapokeo mliyofundishwa, ama kwa maneno, ama kwa waraka wetu.*"

# Hitimisho

Tumepewa Biblia kwa ufunuo.

Tumepewa akili za kibidamu kwa kufikiri na kutii.

Tunapaswa kutumia mambo haya vyema ili kurahisisha hema na tusiruhusu pua la ngamia kuingia ndani.

Hatutumii moyo kana kwamba ni kichwa. Neno la Mungu linapaswa liwe na mamlaka kamili katika maswala ya dini. Mawazo yetu hayapaswi kuwa sawa na ya Mungu. Fikira zake zi juu sana kuliko zetu.

Isa. 55:9, "*Kwa maana kama vile mbingu zilivyo juu sana kuliko nchi, kadhalika njia zangu zi juu sana kuliko njia zenu, na mawazo yangu kuliko mawazo yenu.*"

Kama tukiruhusu pua hili la ngamia katika hema letu, hapo tutaruhusu ngamia atujeruhi.